**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 17 Juni, 2021**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

(a) Ukaguzi Maalum Unaohusu Utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati wa Kuwaapisha Viongozi Wakuu.
(b) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
(c) Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
(d) Ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
(e) Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa mwaka wa Fedha 2018/2020.
(f) Mifumo ya TEHAMA kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Kuweka Usimamizi Mzuri wa Shughuli za Kiislamu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.**

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya Kamati ya PAC Kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

(a) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
(b) Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2020.
(c) Ukaguzi Maalum Unaohusu Utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati wa Kuwaapisha Viongozi Wakuu.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):**

Hotuba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) Kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

(a) Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
(b) Ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.

(c) Mifumo ya TEHAMA kwa Mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.

**III. MASWALI:**

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

132. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Utaratibu wa kukusanya taka za majumbani umebadilika, ikiwa ni pamoja na kuwapangia wananchi siku maalum za kutupa taka katika Manispaa ya Mjini.

(a) Kwa nini Baraza la Manispaa la Mjini hawatengenezi mifuko maalum ya kuhifadhia taka badala ya wananchi kutumia vipolo.

(b) Je, kuwataka wananchi kuziweka taka majumbani kwa siku kadhaa na kutowapatia vifaa vya kuhifadhia taka, hakuwezi kuhatarisha afya za wananchi wetu.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

214. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuleta Sheria nzuri ya Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ili kuleta ufanisi katika manunuzi ya umma. Hata hivyo, mamlaka hiyo imekuwa ikilalamikiwa sana kwa kutotimiza wajibu wake.

(a) Je, tokea kuanzishwa kwa Mamlaka husika ni mara ngapi ripoti zake zimewahi kuwasilishwa katika Baraza lako tukufu kama takwa la Sheria linavyoamrisha.

(b) Kwa kiasi gani Mamlaka imesaidia kuongeza uchumi na ufanisi katika manunuzi ya umma ikilinganishwa na mwaka wa 2005 hadi 2015 na msimu wa 2016 hadi 2020.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

80. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) -

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika jimbo langu la Wingwi eneo la Kije, imeanzishwa skuli ya Sekondari inayoitwa Dkt. Ali Mohamed Shein ambayo imeanza kufanya kazi mwaka huu wa masomo 2021. Wanafunzi wa skuli hiyo wanatoka katika maeneo mbali mbali ya Wilaya ya Micheweni, jambo linalopelekea usumbufu mkubwa kwa wanafunzi hao kuja na kurejea skulini hapo.

Je, Wizara haioni iko haja ya majengo ya kilichokuwa Chuo cha Wazazi Dodeani Wingwi, kuweza kutumika kama mabweni kwa wanafunzi hao.

213. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza Serikali kwa hatua zake za kukuza elimu Zanzibar lakini mnamo mwaka 2016 kulifanyika mabadiliko ya kielimu ambayo yaliondosha somo la dini ya Kiislamu kuwa miongoni mwa Tahasusi za kujiunga na Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundi, hali hiyo imepelekea wanafunzi wengi kutoka Zanzibar kuathirika na kuwagusa hata wanafunzi waliosoma kabla ya mwaka huo.

(a) Je, ni ipi mipaka ya Tume ya Vyuo Vikuu ya Tanzania (TCU) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa katika elimu ya Zanzibar zikiwemo Stashahada na Shahada.

(b) Ni sheria zipi za Zanzibar ziliruhusu maelekezo hayo yasiyo rasmi yaweze kuruhusiwa kuathiri maendeleo ya elimu ya watu wa Zanzibar.

(c) Je, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina wajibu gani kuhakikisha kwamba NACTE na TCU zinatekeleza majukumu yake Zanzibar huku zikielewa kwamba Zanzibar pia ina Wizara dhamana kwa elimu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

163. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa lengo la uwekwaji wa taa za kuongozea vyombo vya moto na waendao kwa miguu barabarani (traffic lights) ni pamoja na kupunguza uwezekano wa kutokea ajali kwa raia. Na kwa kuwa eneo la Machomanne Chake Chake Pemba ni moja ya sehemu hatari mno kutokana na mapishano ya barabara zilivyo.

(a) Je, ni vigezo gani vinavyotumika katika kuweka taa za barabarani (traffic lights) katika barabara mbali mbali ambavyo vimekosekana katika eneo la Machomanne, Pemba.

(b) Je, kutokana na ongezeko la ajali katika eneo hilo, Serikali itachukuwa hatua gani za dharura za kuweka taa hizo kwa haraka ili kuepusha ajali za mara kwa mara katika eneo hilo.

171. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa, bodaboda ni moja ya biashara inayoendelea kukuwa kwa kasi sana ambapo vijana wengi wanaendesha maisha yao kupitia biashara hiyo. Na kwa vile mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika kipindi cha kampeni aliwahi kutembelea kundi hili la bodaboda na kuwaahidi kutatua changamoto zao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuirasimisha biashara hii ili itambulike kisheria.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

180. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Katika vipaumbele vya Bajeti ya mwaka 2020/2021 kwa iliyokuwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, ni kukuza usawa wa kijinsia, kumwezesha mwanamke na kuendeleza mapambano ya kumaliza vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

(a) Je, Wizara inalijuwa suala hili.

(b) Je, Wizara imechukua hatua gani juu ya kumaliza tatizo la udhalilishaji hapa Zanzibar.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

188. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika malengo yake ya mwaka 2020/2021, Kampuni ya Uvuvi ya ZAFICO ilikusudia kushajiisha Jumuiya za Uvuvi kuvua dagaa na samaki wa aina ya jodari kwa ajili ya kusarifu na kusafirisha nje ya nchi.

(a) Je, Wizara yako inaifahamu ahadi hiyo.

(b) Je, ni tani ngapi za jodari zilizovuliwa.

## IV. KAULI YA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

(a) Ukaguzi Maalum Unaohusu Utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati wa Kuwaapisha Viongozi Wakuu.
(b) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
(c) Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
(d) Ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
(e) Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa mwaka wa Fedha 2018/2020.
(f) Mifumo ya TEHAMA kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.

## V. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Kuweka Usimamizi Mzuri wa Shughuli za Kiislamu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

**Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:**

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

**Zanzibar,**
**17 Juni, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**